TANGAZO LA SERIKALI Na. 806 la tarehe 10/11/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA SIMA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Sima ya mwaka, 2023.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Eneo la Upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa eneo

3. Mipango ya jumla na ya kina kwenye eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

JEDWALI

*(Iimetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SV206 yenye majira - nukta 446647.683MS, 9699533.693KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -Mashariki katika uelekeo KZ117º42'00''MS kwa umbali wa kilomita 4.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SV212 yenye majira – nukta 450296.134MS, 9697618.208KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini -Mashariki katika uelekeo wa KS132º45'50''MS kwa umbali wa kilomita 8.59 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SV79 yenye majira - nukta 456606.372MS, 9691782.327KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS91º04'20''KS kwa umbali wa kilomita 8.97 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SV211 yenye majira – nukta 447635MS, 9691950.277KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini -Magharibi katika uelekeo wa KS291º51'50''MG kwa umbali wa kilomita 2.61 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SV210 yenye majira – nukta 445212.786MS, 9692922.347KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ30º00'5''MG kwa umbali wa kilomita 6.76 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SV206 yenye majira – nukta 446647.683Ms, 9699533.693KZ hadi ulipoanzia.

Dodoma,
19 Oktoba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*